East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 4, Issue 1, 2019
ISSN: 1476-4687

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# MATUMIZI YA MAIGIZO KAMA MBINU YA KUFUNDISHA TAMTHILIA KATIKA SHULE ZA UPILI, KAUNTI YA BUNGOMA KUSINI, KENYA

*Inviolata Wekesa Simbi[1*], Dkt. Misiko Wasike[2],*
*Dkt. Deborah Nanyama Amukowa[3] & Dkt. Edwin Masinde[4]*

[1]Chuo Kikuu cha Kibabii, S.L.P 1699 – 50200, Bungoma, Kenya, inviolatasimbi@gmail.com.
[2]Chuo Kikuu cha Kibabii, S.L.P 1699 – 50200, Bungoma, Kenya, dmisiko07@gmail.com.
[3]Chuo Kikuu cha Maseno, S.L.P 3275 – 40100, Kisumu, Kenya, dnanyama@yahoo.com.
[4]Chuo Kikuu cha Kenyatta, S.L.P 43844 – 00100, Nairobi, Kenya, emasinde254@gmail.com.

**Article history:**

*Received: 19 Aug 2019*
*Accepted: 21 Aug 2019*
*Published: 23 Aug 2019*

**Keywords**:

*Maigizo,*
*Tamthilia,*
*Mbinu,*
*Ufundishaji*

## IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kuonyesha matumizi ya maigizo kama mbinu ya kufundisha tamthilia; mfano wa *Kigogo* katika shule za upili, Kaunti ya Bungoma Kusini. Ufundishaji wa somo lolote hujikita kwenye mawasiliano baina ya mwalimu na mwanafunzi. Mbinu za kufundisha huwa viungo muhimu vya kufanikisha mawasiliano haya. Mwalimu ana jukumu la kuteua mbinu mwafaka ya kufundisha. Kuna mbinu mbalimbali mwalimu anaweza kutumia kufundisha tamthilia. Utafiti huu umechagua maigizo kama mbinu ya kufundisha tamthilia. Lengo la utafiti huu lilikuwa kuchunguza iwapo walimu wanatumia mbinu ya maigizo kufundisha tamthilia na wanatumia kwa jinsi gani. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya utendaji inayoshikilia kuwa matini ya kidrama huwasilisha ujumbe vyema zaidi kupitia uigizaji wake katika jukwaa. Utafiti ulilenga shule kumi na sita kati ya shule hamsini na mbili. Walimu wanaofundisha Kiswahili kidato cha tatu na nne pamoja na wanafunzi wa kidato cha tatu na nne ndio waliolengwa. Watafitiwa waliteuliwa kwa kutumia mbinu ya utabakishaji, kinasibu na usampulishaji kimaksudi. Stadi ya utabakishaji ilitumika kuainisha shule katika makundi matatu. Mbinu ya kimaksudi ilitumika kuteua shule tatu za kaunti na walimu wanaofundisha kiswahili kidato cha tatu na nne. Mbinu ya kinasibu ilitumika kuteua shule za kaunti ndogo, shule kumi na mbili na wanafunzi wa kidato cha tatu na nne. Wanafunzi kumi katika kila kidato waliteuliwa, jumla ya wanafunzi mia tatu ishirini walitafitiwa. mbinu zlizotumika kukusanya data zilikuwa hojaji, maswali ya usaili na uchunzaji. Maswali ya usaili yalitumika kukusanya data kutoka kwa walimu. Data ilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa kutumia maelezo, asilimia, picha na majedwali. Matokeo ya utafiti huu yalikuwa kuwa walimu 83% ndio walitumia mbinu ya maigizo kufundisha tamthilia ya *Kigogo*. Utafiti unapendekeza kuwa mbinu za maigizo ambazo hazitumiki pia zitumike ili kuboresha ufundishaji. Vile vile taasisi ya elimu kuandaa semina na warsha za kuwahamasisha walimu kuhusu njia mbalimbali za kutumia maigizo kufundisha. Aidha kila shule iwe na klabu cha maigizo ili kutumika katika ufundishaji wakati wowote.

## UTANGULIZI

Maigizo ni dhana inayotokana na kitenzi ‘iga’. Kwa mujibu wa Kamusi ya TUKI (2004), neno *iga* ni kutenda jambo kama anavyofanya mwingine. Kulingana na Mulokozi (1989), maigizo ni sanaa inayotumia watendaji kuiga tabia au matendo ya watu na viumbe wengine ili kuburudisha na kutoa ujumbe fulani. Kulingana na Wanjala (2011), maigizo ni masimulizi yanayoambatana na matendo kwenye jukwaa mbele ya hadhira. Anaendelea kusema kuwa maigizo hufanywa kwa madhumuni ya kuwasilisha ujumbe fulani katika jamii kwa njia ya matendo. Maigizo ni utanzu wa fasihi simulizi ambao hutumia mazungumzo ambayo yanaambatana na matendo ili kuwasilisha ujumbe fulani kwa hadhira. Katika maigizo, wahusika watendaji huiga matendo na tabia za watu katika maisha halisi ili kuwasilisha ujumbe fulani kwa hadhira maalum. Maigizo huwa na mahali maalum pa kuwasilishia matendo yao kwa hadhira yaani jukwaa. Japo maigizo ni utanzu unaojisimamia katika fasihi, unaweza kutumika kama mbinu ya kufundisha tamthilia teule katika shule za upili.

Tamthilia ni fani ya fasihi iliyokusudiwa kutendwa jukwaani kwa ajili ya hadhira Fulani (Mulokozi, 1996). Mulokozi anaendelea kueleza kuwa istilahi tamthilia inatokana na neno mithali ambalo lina maana ya mfano au ishara ya kitu. Hivyo katika tamthilia kitu kimoja humithilishwa au kufananishwa na kitu kingine. Mwandishi hutunga tamthilia kwa kuiga mambo yanayotendeka katika maisha halisi.

Ufundishaji ni mchakato unaohusisha mawasiliano kati ya mwalimu na mwanafunzi. Ili ufundishaji utekelezwe vyema, lazima pawe na mawasiliano mazuri kati ya mwalimu na mwanafunzi. Mbinu za kufundisha huwa viungo muhimu vya kufanikisha mawasiliano haya. Kuna njia nyingi ambazo mwalimu anaweza kutumia kufundisha tamthilia. Kwa hivyo ni jukumu la mwalimu kuteua njia mwafaka ya kuwasilisha mafunzo kwa mwanafunzi. Katika kipindi hiki cha sasa mbinu za mwelekeo mseto ni mwafaka kutumika katika ufundishaji kwani humshirikisha mwanafunzi katika ufundisha. Maigizo ni miongoni mwa mbinu za mwelekeo mseto. Aidha, waandalizi wa mitaala katika elimu wanapendekeza matumizi ya mbinu zinazompa mwanafunzi fursa ya kushiriki katika mchakato wa ufundishaji. Mbinu ya maigizo ni mojawapo ya mbinu zinazompa mwanafunzi fursa ya kushiriki katika mchakato wa ufundishaji. Utafiti huu ulilenga kuonyesha iwapo walimu hutumia mbinu ya maigizo kufundisha tamthilia; mfano wa *Kigogo* na wanaitumia namna gani?

## UHAKIKI WA MAANDISHI

Bigambo (1987) alitafiti kuhusu uigizaji katika muktadha wa majaribio ya ufundishaji na kupata kuwa maigizo yana nafasi ya kuupa ufundishaji uhai na hivyo kuwa kivutio kwa wanafunzi. Gituku (1990) alitafiti juu ya maigizo ya kienyeji ya watoto nchini Kenya na dhima yake katika ufundishaji. Mtafiti alibaini kwamba maigizo yanaweza kutumika ili kuboresha ufundishaji katika shule za msingi kwa sababu huleta uhai darasani. Utafiti wa Owino (2011) ulitathmini matumizi ya TEKNOHAMA katika ufundishaji wa Riwaya ya Kiswahili katika shule za upili wilayani Kisumu Magharibi. Alitambua kuwa walimu wachache walitumia mbinu ya TEKNOHAMA kufundisha riwaya ya Kiswahili. Aidha mbinu hii inakabiliwa na changamoto anuai kama vile; ukosefu wa pesa, matumizi ya TEKNOHAMA katika kwa shughuli zisizowiana na ufundishaji na ukosefu wa miundo misingi inayohitajika kuimarisha matumizi ya TEKNOHAMA katika ufundishaji wa riwaya. Barasa (2012) alichunguza kuhusu utendaji katika ufundishaji wa ngano katika shule za upili nchini Kenya. Alibaini kwamba mbinu ya utendaji ikitumika katika ufundishaji wa ngano darasa huchangamka. Mbinu ya utendaji huchangia kuleta uhalisia darasani. King’ora (2014) alitafiti kuhusu utendaji katika tamthilia za *Sudana* na *Kimya Kimya Kimya*. Alitaka kubaini iwapo tamthilia za *Sudana* na *Kimya Kimya Kimya* zilizingatia kigezo kikuu cha matini za kidrama ambacho ni uwezo wa kuwasilishwa jukwaani au zilikuwa na majibizano ya usemi tu. Mtafiti alibainisha kwamba tamthilia hizo zilikuwa na vipengele ambavyo vilizisaidia kuwa na uwezo wa kuwasiliswhwa jukwaani. Tafiti hizi zinalenga mbinu za ufundishaji na tamthilia lakini hazijashughulikia maigizo kama mbinu ya kufundisha tamthilia.

## MBINU ZA UTAFITI

### Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika Kaunti ya Bungoma Kusini nchini Kenya katika shule za upili. Eneo hili lina jumla ya shule hamsini na mbili (52) na walimu sitini (60) wanaofundisha somo la kiswahili.

### Sampuli Lengwa

Kiwango katika sampuli kamili hutegemea vigezo vya idadi lengwa ya utafiti na makisio anayokusudia mtafiti (Cooper, 1998). Sampuli lengwa ilikuwa walimu wanaofundisha fasihi kidato cha tatu na wanafunzi wa kidato cha tatu na nne. Walimu waliteuliwa kwa sababu ndio wateuzi na waelekezi wakati wa matumizi ya mbinu za kufundisha. Mtafiti alichagua wanafunzi wa kidato cha tatu na nne kwa kuwa ndivyo viwango vinavyofundishwa vitabu viteule vya fasihi. Walimu kumi na nane (18) ndio waliolengwa katika utafiti na shule kumi na sita (16). Wanafunzi kumi (10) waliteuliwa katika kila kidato jumla ya wanafunzi mia tatu ishirini (320) walitafitiwa.

### Usampulishaji

Mtafiti alitumia uteuzi wa utabakishaji, kinasibu na usampulishaji kimakusudi ili kupata watafitiwa. Yuko na Owen (2005) wanasema kuwa utabakishaji husaidia kueleza tofauti za kisifa zinazopatikana miongoni mwa matabaka tofauti. Stadi hii ilitumika kwa madhumuni ya kuwakilisha washiriki katika kila tabaka linalopatikana katika sampuli lengwa. Utabakishaji ulitumiwa kuainisha shule za eneo hili katika makundi matatu: shule za kaunti za kiwango cha juu, shule za kaunti za kiwango cha kati na shule za kaunti za kiwango cha chini. Mbinu ya kimakusudi ilitumiwa kuteua walimu wa Kiswahili wa kidato cha tatu na cha nne kwa sababu wao ndio hupanga na kuelekza mchakato mzima wa ufundishaji wa somo. Aidha ilitumika kuteua wanafunzi wa kidato cha tatu na cha nne kwa kuwa mara nyingi vitabu viteule hufundishwa katika vidato hivi. Pia, mbinu hii ilitumika kuteua shule tatu (3) za kiwango cha juu na shule moja (1) ya kaunti kiwango cha kati. Usampulishaji wa kinasibu ulitumika kuteua shule za kaunti za kiwango cha chini shule kumi na mbili (12) na kuchagua wanafunzi kumi katika kila kidato.

### Mbinu za Kukusanya Data

Mtafiti alitumia maswali ya usaili, hojaji na uchunzaji kama vifaa vya kukusanya data. Maswali ya usaili yalitumika kupata data kutoka kwa walimu, ratiba ya uchunzaji ilitumika kukusanya data kutoka darasani wakati wa kipindi. Hojaji nazo zilitumika kusanya data kutoka kwa wanafunzi.

## MATOKEO

### Maigizo katika Ufundishaji wa Tamthilia

Maigizo yanaweza kutumika kama mbinu ya kufundisha vipengele vya tamthilia. Maigizo yana sifa ambazo zinaweza kutumika kuchambua vipengele vya tamthilia kwa njia ya kusisimua wanafunzi. Sifa hizi huzifanya tamthilia kuwa na uhalisia darasani. Njogu na Chimerah (1999) wanabainisha fani muhimu katika uchanganuzi wa tamthilia. Fani hizo ni jukwaa, wahusika maleba, matendo au ishara za wahusika. Mtafiti alitaka kujua jinsi maigizo yalivyotumika kufundisha tamthilia ya *Kigogo*. Utafiti huu ulizingatia mihimili miwili ya nadharia ya utendaji; mhimili wa la tukio la utendaji na mhimili wa jukwaa.



***Picha 1***

Katika **picha 1** ni kikundi hai cha kuigiza cha *'Luwaza Arts Production'* kikiigiza onyesho la tatu tendo la kwanza. Jukwaa limepangwa kudhihirisha mandhari ya afisi vilevile. Maleba ya waigizaji yanadhihirisha hali ya maisha ya waigizaji. Kuna

vihusika ambavyo vinadokeza ujumbe juu ya hali ya maisha na uhusiano wa wahusika wa onyesho hilo.



***Picha 2***

**Picha 2** waigizaji wanaigiza onyesho la kwanza tendo la kwanza. Jukwaa linadhihirisha mandhari ya karakana. Maleba ya waigizaji yabainisha hali ya maisha ya umaskini. Kuna vikombe kwenye meza kudhihirisha kwamba uhusiano uliopo kati ya wahusika hao ni wa karibu sana.



***Picha 3***

**Picha 3** ni kanda ya video. Jukwaa la kanda limepangwa kudhihirisha mandhari ambayo ni ya karakana.Jukwaa vilevile lina vihusika vinavyobainisha aina ya kazi inayofanywa na waigizaji. Vihusika vinavyopatikana katika jukwaa hili vinadokeza aina ya kazi wanayojihusisha nayo. Wanafanya kazi ya uchongaji ambayo inawapa riziki yao. Vihusika hivyo ni mbao.



***Picha 4***

**Picha 4** ni uigizaji wa kikundi cha '*Luwaza Arts Production'*. Wanafunzi wanatazama uigizaji wa tamthilia ya *Kigogo*.

**Maigizo katika Ufundishaji kwa Mujibu wa Walimu**

*Jedwali 1: Vipengele vya maigizo vilivyotumika katika ufundishaji wa tamthilia ya Kigogo kwa mujibu wa walimu*

| | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Jukwaa | 15 | 83 |
| Maleba | 10 | 55 |
| Mandhari | 6 | 33 |
| Miondoko na Ishara | 8 | 44 |
| Utendaji | 10 | 55 |
| Vihusika | 2 | 11 |

Matokeo yalionyesha kuwa walimu kumi na tano (15) kati ya walimu kumi na nane (18) walikiri kutumia jukwaa katika kufundisha tamthilia ya *Kigogo*. Walimu hawa walisema kuwa jukwaa lilitumika kupambanua maudhui na kuainisha wasifu wa wahusika katika kila onyesho. Kila onyesho huwa na jukwaa maalum ambalo hudhihirisha ujumbe fulani uliokusudiwa kuwasilishwa na mwandishi.

Walimu wote wanashadidia kwamba hutumia vikundi hai vya waigizaji kufundisha. Walimu sita (6) wanadai kwamba hualika kikundi hai cha 'Jicho Four' shuleni ambao huigiza wanafunzi wakitazama. Walimu tisa (9) nao walisema kuwa huwapeleka wanafunzi wao kujumuika na wenzao katika shule zilizoalika vikundi hai vya uigizaji kwa mfano kikundi cha 'Jicho Four'. Kikundi cha 'Jicho

Four" hupanga jukwaa kulingana na maelekezo ya mwandishi katika onyesho husika. Jukwaa hilo hudhihirisha ujumbe kutokana na rangi ya vitambaa vilivyotumika na vihusika vilivyopangwa hapo. Wamitila (2002) anashadidia kwamba jukwaa huwa na dhima ya kudokeza mandhari, maleba, matendo, ujaji na uondokaji wa wahusika. Kwa hivyo jukwaa huwa na athari kubwa kwa kazi nzima ya tamthilia. Kupitia kwayo maudhui na sifa za wahusika katika onyesho husika zinabainika. Walimu walidai kuwa pia walitumia kanda za video kudhihirisha jukwaa la kila onyesho na kuwaelekeza wanafunzi kulingana na jukwaa hilo.

Walimu kumi (10) walithibitisha kuwa hutumia maleba kufundisha vipengele vya maudhui na sifa za wahusika. Waigizaji wanapoingia kwenye jukwaa, maleba waliyojivika yanatumiwa kubainisha maudhui yaliyolengwa na mwandishi pamoja na tabia na mienendo ya mhusika anayewakilishwa katika uigizaji husika. Walimu wawili (2) kati yao walikiri kuwa hutumia wanafunzi wenyewe kufaragua maleba ya wahusika mbalimbali. Wanafunzi huvaa maleba kuwakilisha wahusika wa tamthilia ya *Kigogo* wakati wa kipindi. Walimu nane (8) walitumia vikundi maalum vya uigizaji kuonyesha jinsi maleba yalivyotumika kuwasilisha ujumbe. Walimu wanne (4) nao walitumia kanda za video.

Walimu nane (8) walitumia miondoko na ishara kufafanua hasa sifa za wahusika na maudhui. Walimu hawa walitumia vikundi maalum vya uigizaji. Walimu walibainisha jinsi waigizaji walivyoigiza kwa kuiga miondoko ya wahusika wa tamthilia ya *Kigogo.* Walimu Kumi (10) walithibitisha kutumia utendaji kufundisha maudhui na sifa za wahusika. Walimu wote walitumia vikundi maalum waliotenda mbele ya jukwaa maonyesho mbalimbali ya tamthilia ya *Kigogo*. Kupitia kwa utendaji wa waigizaji, tabia na mienendo ya wahusika inabainika, aidha mawazo ya mwandishi yanadhihirika. Kando na vikundi maalum vya uigizaji, walimu walitumia kanda za video kuonyesha utendaji wa waigizaji wakati wa kipindi huku wakiwaelekeza. Walimu wawili (2) ndio walitumia vihusika kufafanua maudhui na wasifu wa wahuska. Vihusika ni vifaa vyenye maumbo yanayoonekana. Walimu hao walidai kuwa walitumia vihusika kuweka wazi tabia na kuashiria wazo. Kipengele hiki kilionyweshwa kupitia kwa jukwaa. Walimu hawa walitumia vikundi hai na kanda za video kufundisha.

**Maigizo katika Ufundishaji wa Tamthilia kwa Mujibu wa Wanafunzi**

*Jedwali 2: Matumizi ya maigizo katika ufundishaji wa tamthilia kwa mujibu wa wanafunzi*

| | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| Jukwaa | 200 | 63 |
| Maleba | 140 | 44 |
| Mandhari | 100 | 31 |
| Miondoko na ishara | 80 | 25 |
| Utendaji | 180 | 56 |

Wanafunzi mia mbili (200) ambao ni asilimia sitini na tatu (63%) walithibitisha kuwa jukwaa lilitumiwa na walimu kufundisha maudhui na sifa za wahusika. Wanafunzi mia moja hamsini (150) kati ya mia mbili (200) walikiri kwamba hutumia vikundi hai vya kuigiza kufundisha tamthilia ya *Kigogo.* Wanafunzi mia moja na kumi (110) kati ya wanafunzi mia mbili (200) walidai kuwa walimu wao walitumia kanda za video kudhihirisha jukwaa la kila onyesho. Wanafunzi mia moja arobaini (140) ambayo ni asilimia arobaini na nne (44%) waliafiki kwamba walifundishwa maudhui na sifa za wahusika kupitia kwa uigaji wa maleba ya wahusika wa tamthilia ya *Kigogo.* Wanafunzi arobaini (40) walidai kwamba walimu walitumia wanafunzi wenzao kufaragua maleba ya wahusika wa tamthiliani na kuyatumia wakati wa kipindi. Wanafunzi asilimia themanini (80%) wanakubali kwamba walimu wao walitumia vikundi hai vya kuigiza na kanda za video kudhihirisha maleba yanayoigwa kutoka kwa tamthilia ya *Kigogo*.

Wanafunzi mia moja (100) ambao ni asilimia thelatini (30%) walikiri kuwa walifundishwa kipengele cha maudhui na cha sifa za wahusika kwa kutumia mandhari yaliyowekwa katika hali halisi kupitia kwa kanda za video na uigizaji wa vikundi hai. Asilimia hamsini na sita (56) ya wanafunzi ambao ni mia moja themanini (180) walionyesha kwamba utendaji wa waigizaji ulitumiwa sana katika kufundisha vipengele vya tamthilia ya *Kigogo.* Wanafunzi mia moja ishirini (120) kati ya mia moja themanini (180) walisema kuwa walimu walivialika vikundi hai vya kuigiza shuleni.

Wanafunzi sitini (60) kati ya mia moja themanini (180) walipelekwa na kujumuika pamoja na wanafunzi wenzao katika shule moja ambayo iliteuliwa na kikundi hai kuigizia tamthilia ya *Kigogo.* Aidha, wanafunzi mia moja ishirini (120) walikiri kuwa walichambua tamthilia ya *Kigogo* kupitia utendaji wa waigizaji katika kanda za video. Asilimia ishirini na tano (25%) ya wanafunzi ambao ni themanini (80) waliafiki kwamba walimu walitumia miondoko na ishara za wahusika kufunza vipengele vya tamthilia ya *Kigogo*.

**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

Lengo la makala haya lilikuwa kuonyesha matumizi ya maigizo kama mbinu ya kufundisha tamthilia mfano wa *Kigogo*. Utafiti ulibaini kwamba mbinu ya maigizo inatumika katika kufundisha tamthilia japo walimu kumi na tano (15) ambao ni asilimia themanini na tatu (83%) ndio hutumia. Ilibainika wazi kutokana na matokeo kuwa vikundi hai vya kuigiza na kanda za video zinatumika kwa wingi kufudishia tamthilia ya *Kigogo*. Walimu watatu (3) inayowakilishwa na asilimia (17%) hawatumii mbinu ya maigizo kufundisha. Makala haya yanalenga kuboresha somo la Kiswahili kwa kuleta uhalisia darasani na kushirikisha wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji.

Makala haya yanapendekeza kuwa mbinu za maigizo ambazo hazitumiki pia zitumike ili kuboresha ufundishaji. Mbinu kama vile drama ya wanafunzi; vile vile utafiti unapendekeza kila shule iwe na klabu ya maigizo ili itumike katika ufundishaji shuleni mwao wakati wowote wanaopenda. Pia, taasisi ya elimu iandae semina na warsha za kuwahamasisha kuhusu mbinu mbalimbali za kutumia maigizo kufundisha.

**MAREJELEO**


Barasa, O. P. (2012). *Utendaji katika Ufundishaji wa Ngano kwenye Shule za Upili Nchini Kenya*. Tasnifu ya Uzmili Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Masinde Muliro.

Bigambo, O. (1987). *Uigizaji katika Muktadha wa Majaribio ya Ufundishaji*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi.

Copper, H. (1998). *Aids to Teaching and Learning.* New York: Pergamon Press.

Gituku, N. (1990). *Maigizo ya Kienyeji ya Watoto Nchini Kenya na Dhima yake katika Ufundishaji*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta.

King’ora, N. (2014). *Utendaji katika Tamthilia za Sudana na Kimya Kimya Kimya*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mulokozi, M .M (1996). *Utangulizi wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: TUKI

Mulokozi, M. M. (1989). Tanzu za Fasihi Simulizi.Mulika, *21,* 1-24.

Njogu, K.na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Foundation.

Owino, A. O. (2011). *Tathmini ya Matumizi ya Teknolojia katika Ufundishaji wa Riwaya ya* Kiswahili katika Shule za Upili Wilayani Kisumu Magharibi: Tasnifu Ya Uzamili Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro.

TUKI. (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (Toleo la pili)*. East Africa: Oxford University Press.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: misingi na vipengele vyake.* Nairobi: Focus Publication.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus publication

Wanjala, S. F. (2011). *Kitovu cha Fasihi Simulizi kwa Shule vyuo na Ndaki.* Mwanza: Serengeti Educational Publishers Ltd.

Wilson, E. (1998). *The Theatre Experience.*New York: The McGraw Hill Companies.

Yuko, W. na Owen, D. (2005). *A Handbook for Beginning Researcher*. Otiona press and Publication.